# Kikale cha Kifo kama Mbinu ya Utunzi katika Fasihi ya Kiswahili

*Ezra Nyakundi Mose*[1] na *Samuel M. Obuchi*[2]
[1]*Chuo Kikuu cha Kisii*
[2]*Chuo Kikuu cha Moi*

**Ikisiri**

**Makala haya yanachunguza tukio la hatima ya maisha ya kifo ambalo kwa muda mrefu limekuwa likidhihirika na kutumiwa na watunzi katika kazi za sanaa hususani tamthilia. Kifo ni taashira kongwe ambayo imekuwepo katika kazi za sanaa za jamii zote ulimwenguni na katika vizazi na ustaarabu wa nyakati mbalimbali. Kifo kama kikale kimekuwa kikijitokeza mara kwa mara katika kazi za sanaa kwa njia ya kujirudia rudia kiasi kwamba kinajibainisha kama motifu ya utunzi wa kazi za fasihi inayoathiri muundo na dhamira za kazi hizo. Matokeo ya uchunguzi yanafafanua matumizi ya kifo kama mbinu ya utunzi wa tamthilia ya Kiswahili na kudhihirisha kifo kama kikale kinachojirudiarudia katika kazi za fasihi. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhakiki wa vikale iliyoasisiwa na mtaalamu Northrop Frye (1957) kutoka Kanada.**

**Maneno Muhimu:** *Kifo, kikale, tanzia, tamthilia ya Kiswahili*.

**Utangulizi**

Matumizi ya kifo kama mbinu ya utunzi katika fasihi yalidhihirika mwanzo kabisa katika fasihi ya Ugiriki ya wakati wa urasimi mkongwe. Misingi ya matumizi ya kifo katika fasihi ya Kigiriki ilimwezesha mwanafalsafa mkongwe, Aristotle, kuunda mihimili ya Nadharia ya tanzia. Matumizi ya tukio la kifo kama mbinu ya utunzi wa kazi ya fasihi ndio hukamilisha kazi za fasihi za aina ya tanzia ambapo kifo ndio tanzia yenyewe. Aristotle kama mwanafalsafa, mwananadharia na mwahakiki wa awali kabisa, ndiye wa mwanzo kufafanua matumizi ya kifo katika fasihi kama mbinu ya utunzi katika kitabu chake cha *Poetics*. Wanafalfasa na wataalamu wengine wa baadaye ambao pia wamerejelewa katika makala haya wameegemeza maelezo yao katika mawazo ya Aristotle kuhusu tanzia. Katika makala haya tumeangazia mikondo ya matumizi ya tukio la kifo kama mbinu ya utunzi wa tamthilia za Kiswahili na kazi zingine za fasihi kwa jumla ili kudhihirisha kifo kama kikale kinachojirudiarudia katika kazi za fasihi.

**Mitazamo na Mbinu za Matumizi ya Kifo katika Fasihi**

Kitika matumizi ya kawaida, kifo ni dhana inayorejelea hali ya kukoma kabisa katika matumizi ya viungo muhimu vya mwili wa kiumbe au kitu chenye uhai (Merriam, na C. Co 1971 na TUKI, 1981). Tukio la kifo huashiria mwisho wa maisha ya mtu, mnyama, mti au kitu. Kifo, vilevile, hurejelea au huwa na maana ya tanzia. Dhana ya kifo, vilevile, ni kisawe cha tanzia. Nkwera (1978) anaeleza kwamba tanzia ni tangazo la kifo au habari ya kifo. Hivyo, kifo au tanzia ni dhana zinazorejelea mwisho wa maisha. Katika sanaa, hasa fasihi, michezo ya tanzia husheheni visa, vituko na migogoro yenye kuendana na masikitiko, maanguko na hasara kwa mhusika mkuu na jamii kwa ujumla. Aristotle aliuona utanzu huu kama "mwigo" au uigizaji wa tendo ambalo lina udhati, ukamilifu, ubora au ukuu fulani. Tendo hilo lazima liwe na uwezo wa kuwaathiri watazamaji na kuwafanya waingiwe na huzuni pamoja na uwezo wa kuzitakasa hisia za woga au huzuni katika kile alichokiita "mtakazohisia". Tamthilia ya *Mfalme Edipode* iliyoandikwa na Sofokile na ambayo ilitafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na Mushi (1971) nni mfano mzuri wa wa tanzia.

Sage (1962) anaeleza kwamba tukio la kifo hutumiwa kiishara katika utunzi wa kazi ya fasihi kuwakilisha mwisho wa mwongo wa aina fulani wa kitengo cha maisha. Kifo cha mhusika kinapotokana na kafara au wakati mhusika anajitia kitanzi katika kazi ya fasihi baada ya kushindwa kuvumilia na kuhimili misukosuko ya maisha, huwakilisha maana ya ndani inayotumika kitaswira. Muindi (1990) anaeleza kwamba mhusika anaweza kufishwa na msanii kisanaa kwa kumtowesha

kutoka kwa mfululizo wa visa na wakati mwingine msanii anaweza kumruhusu mhusika kufa katika hali za maisha ya kawaida.

Kifo cha wahusika katika mchezo wa kuigiza huwa na maana ya kijazanda (Indagasi, 1991). Kifo cha wahusika katika kazi ya fasihi ni mbinu ya utunzi inayotumiwa na watunzi wa kazi za sanaa kwa nia na dhamira mahususi. Kifo au vifo vya aina hiyo katika kazi ya sanaa husheheni dhima fulani ya kazi hiyo na hutumiwa kama mbinu ya ujenzi wa mchezo huo. Riwaya ya Wole Soyinka ya *The Swamp Dwellers* ina wahusika ambao walikuwa "nusu hai na nusu wafu". Hivyo, walivyokuwa wakiishi pangoni chini ya ardhi ilhali katika uso wa dunia, kila kitu kilikuwa kimekauka na kufa. Wahusika hawa wakijipata katika pango chini ya ardhi ambapo hakuna uhai, wanapata hali ya utulivu. Wole Soyinka anatumia hali hii tatanishi kwa dhamira ya kumwonyesha msomaji hali ya kutokuwa na matumaini kwani kifo kilikuwa kinawinda na kuangamiza chochote kilichokuwa na uhai. Ubunifu wa mtunzi unajenga taashira za kifo kinachozunguka katika uso wa dunia na kuwinda viumbe kwa kuwaua jinsi vilivyofanya vidimbwi vya maji katika kiza hicho. Vidimbwi vya maji katika *The Swamp Dwellers* vina jazanda ya kifo. Mhusika Makuri anasema:

> Huu ndio mwisho. Huu ndio umbali ambao binadamu anaweza kufika …
> (*The Swamp Dwellers* (Uk - 89)

Matumizi mengi ya kifo katika kazi za fasihi hudhihirika katika aina ya kazi inayoitwa tanzia. Kulingana na Roderick (1986:120), Aristotle alifafanua tanzia kwa kusema kwamba:

> Tanzia ni uigizaji wa kitendo ambacho ni nyeti na kilichojaa visa
> vinavyozua huruma na woga. (*Tafsiri ya mtafiti*)

Kifo, katika sanaa, hutokana na makosa, uhalifu au dhambi inayosababishwa na mhusika wa tanzia au jamii yake. Hatimaye, mhusika huyo hupata mateso yenye uchungu mwingi na adhabu ambayo inapita kiwango cha uhalifu au kosa lake asilia. Katika kuwachora wahusika katika kazi zao, wasanii, wakati mwingine, huwafanya wahusika fulani kutoweka ghafla kutoka kwa mfululizo wa visa. Mtunzi anaweza kuwaua wahusika kupitia kwa njia mbalimbali: kifo cha kawaida, ajali, kuuliwa na watu wengine, kujiua wenyewe. Hizi ni baadhi ya mbinu ambazo msanii anaweza kupendelea katika kuitekeleza azma yake. Kifo, mauaji au kafara kama inavyodhihirika katika maelezo ya Aristotle kuhusu tanzia, husababisha athari ya woga na huruma katika mioyo ya watazamaji wa mchezo wa kuigiza.

Samuel Beckett akinukuliwa na Catherine Obianuchu (1984) anafafanua kwamba msanii, kupitia kwa wahusika wake, anaweza kuyadhihirisha maisha ya wahusika kama yenye kujaa utupu tele na, kwamba, maisha ya mwanadamu yataishia hapa:

> "Siku moja tulizaliwa na siku moja tutakufa. Siku moja, wakati mmoja, …
> walizaa huku miguu ikipanuka kuelekea kaburini. Mwangaza
> huwaka na kuzimika tena, hivyo kuleta usiku kwa mara nyingine".
> (*Waiting for Godot,* uk 89). (*Tafsiri yetu).*

Ingawa kifo ni tukio la kawaida ambalo linaweza kumpata mtu yeyote, kifo cha kitanzia humpata mhusika au wahusika maalumu katika kazi ya sanaa. Mhusika wa tanzia ni "kiungo cha kati" ambaye huja kati ya miungu na watu wa kawaida. Mhusika wa tanzia, vilevile, ni mtu ambaye ni mwadilifu na mwenye kuandama haki lakini ambaye, kwa bahati mbaya, kifo chake hakitokani na uovu wake bali kwa sababu ya makosa ya uamuzi fulani unaofanywa na wale walio katika mamlaka na wanaotaka kutetea mamlaka yao au kudumisha hali zao fulani za maisha zinazohatarishwa. Hivyo, kifo huwa mbinu mwafaka ya kisanaa ya kuchunguza migogoro kati ya watu wa kawaida wanaoonewa na wale wanaong'ang'ania au walio katika mamlaka.

Matumizi ya kifo katika kazi za sanaa huwa ya kujirudiarudia katika kazi mbalimbali na usawiri wake ni wa namna ya vikale. Samuel Beckett (amekwishatajwa), humwona binadamu kama kiumbe kisichokuwa na uwezo wa kubadilisha hatima yake. Kulingana na Beckett, binadamu ni mtenda dhambi. Hivyo, hana nafasi ya kujikomboa na hawezi kujiokoa kwani maisha ni safari ya masafa mafupi. Lililo dhahili ni kwamba, dunia ni kaburi na mwisho wake ndio mwanzo.

Diomedes katika karne ya nne baada ya kuzaliwa Masiha, akifafanua dhana ya tanzia alieleza kuwa ni masimulizi kuhusu mikasa inayowapata mashujaa au wahusika ambao ni binadamu wa kawaida na wale ambao ni nusu miungu. Isidore wa Seville aliyeishi kati ya karne ya sita na saba baada ya kuzaliwa Masiha (Cuddon1977), naye alieleza kwamba kifo katika tanzia hujumuisha hadithi za kuhusunisha kuhusu mataifa na wafalme wake. John wa Garland, katika karne ya 12 baada ya kuzaliwa masiha, naye alieleza kifo cha kitanzia kama shairi lililoandikwa kwa mbinu ya upeo kuhusu matendo maovu na ya kuaibisha. Aidha, tanzia ni shairi ambalo huanzia kwa furaha na kukamilika kwa majonzi.

**Kifo kama Mbinu ya Utunzi**

Katika kufafanua umuhimu wa kifo kama mbinu ya uandishi wa kazi za Fasihi, Bw. Philip Sidney alielezea kifo katika kazi ya fasihi kama mbinu bora ya kufungulia na kudhihirisha vidonda vya ajabu na kuweka wazi athari mbaya ya vidonda hivyo vilivyofunikiwa (Cuddon; amekwishatajwa). Kifo au tanzia huwa na wajibu wa kuwafanya wafalme au watu wenye mamlaka kujiepusha na ukatili, ambapo walio wakatili kuandama mienendo ya kimaadili. Visa vya kitanzia huwa kama fundisho kwa watu kujisaili hali na mitazamo yao ya maisha kwa lengo la kujirekebisha.

Uigizaji wa tanzia umekuwa mbinu ya kusawiri visa na mikasa katika jamii na hatimaye kifo ambacho huwafika binadamu wenye vyeo, mamlaka na nafasi zao. Kwa mfano, Antigone, Romeo na Juliet, Antony na Cleobatra, Hamlet kati ya wahusika wengine wametumiwa na wasanii kuwasilisha visa na mikasa iliyoko katika jamii zao. Kinachowafanya wahusika hawa kusombwa na tanzia ni kwamba wanazo sifa fulani hadimu za ubora, utukufu na mapenzi, sifa ambazo hazipatikani kwa kawaida. Aidha, wanao uadilifu na vipawa fulani hadimu ambavyo huwatofautisha au kuwatenganisha na watu wa kawaida ambao hatima yao ni kifo. Licha ya kuwa na sifa hizi za ubora, hawawezi kukombolewa kutokana na kifo kama Cuddon anavyomnukuu Anouilh katika tamthilia ya *Antigone* akisema:

> "…Mashine hiyo iko katika hali timamu, imetiwa mafuta tangu wakati uanze,
> na inazunguka bila kukwama au kusuguana. Kifo, jinai na huzuni vinakuja kwa mikiki na vishindo: vitu hivi vinasonga mbele katika wimbi kubwa la majonzi na upweke… Kifo ni nadhifu, kinapumzisha na hakina kosa…"

Kifo ni mkasa unaowajia wahusika ambao wanawakilisha kwa njia fulani yale makosa na upungufu unaopatikana katika binadamu wa kawaida katika jamii mahsusi kama fidia ya upungufu wao. Kifo ni ule mkasa unaowafika watu wengine. Mtu au mhusika akifa akiwa wa hadhi kubwa ndivyo mkasa nao huwa mkubwa. Matumizi ya kifo katika kazi ya fasihi ni jinsi ya kulalamika. Hivyo, kifo ni kilio cha haki, ni malalamiko, hasira au uchungu dhidi ya kinachosababisha hali hiyo ya mateso. Kifo ni kilio kuhusu hali ya tanzia ambayo kwayo shujaa wa tanzia hujipata. Kisa kuhusu maisha na kifo cha Kristo kilikuwa na misingi ya tanzia hasa katika kipengele cha kifo chake kutohebukika. Kifo chake kilitabiriwa kitambo na manabii mbalimbali katika Agano la Kale. Kwa kushiriki katika mateso, uchungu na woga wa shujaa wa tanzia, mtazamaji wa mchezo wa tanzia kwa maoni ya Aristotle huhisi huruma na woga na hivyo hutakasika. Tanzia au kifo cha wahusika wa mchezo wa kuigiza chaweza kumfanya mtazamaji alie lakini baada ya kutokwa na machozi hujihisi vyema tena. Hivyo kifo ni hali ya kisaikolojia inayoigizwa kisanaa kuwaboresha watu kimaadili.

**Mabadiliko katika Muundo wa Tanzia**

Wagiriki ndio walikuwa wa kwanza kuandika visa vyenye matumizi ya kifo na ni kwa misingi ya kazi walizoziandika ambapo Aristotle alibuni mihimili ya tanzia katika fasihi. Lakini kwa ajili ya kujihusisha na usomi wa Aristotle, kwa nia mbaya au nzuri nadharia yake ya tanzia ilinyumbuliwa na wasomi wa baadaye. Unyumbuaji wa wasomi hawa ulibadilisha mihimili ya nadharia ya Aristotle ili kuifanya ichukuane na kuafiki mienendo ya aina za tanzia zingine katika matumizi yao.

Mwishoni mwa karne ya kumi na tisa kulishuhudiwa mabadiliko makubwa katika muundo wa tanzia na maudhui yake. Kazi nyingi zilianza kuonyesha mikasa ya magonjwa, ukichaa, urithi mbaya, na uozo mwingine katika jamii. Taaashira ya kitanzia ikasawiri jamii ambayo imekuwa gonjwa

kiroho, iliyooza kimaadili, najisi na fisadi. Hivyo, tanzia ikaanza kuonekana kama mbinu ya kisanaa ya kueleza na kutoa fumano la hali ya binadamu katika maisha yake kwa mujibu wa jamii yake, mtazamo wake kuhusu maisha na wajibu wake katika mtazamo huo. Senkoro (1983) anaeleza ya kwamba yale anayoyaandika msanii hayazuki hivi hivi tu kutoka ombwe tupu bali yanahusishwa na hali halisi za kisiasa, kiuchumi na kitamaaduni zinazoibuka kutokana na mfumo wa jamii inayohusika. Msanii kama mmoja katika jamii yake huchota maudhui na dhamira zake kutoka kwa mazingira alimokulia. Izingatiwe ya kwamba jinsi binadamu hukua na kubadilika kila uchao ndivyo maudhui nayo katika kazi za fasihi huenda yakibadilika. Katika kipindi cha hivi sasa, visa vya tanzia vimebuniwa kumulika mateso, mikasa na udhalimu unaofanyiwa watu wa kawaida, ukatili, maovu ya ukoloni, unafiki, unyanyasaji, miongoni mwa maswala mengine jambo ambalo ni kinyume na masuala ya tanzia ya jadi iliyoangazia wahusika wafalme, malkia na watoto wao tu. Vilevile, katika wakati wa hivi sasa watu wote wakiwemo masikini, wakulima, makahaba, wezi, wachuuzi, vilema, wagonjwa na watu wengine ambao walitazamwa na jamii kuwa viumbe duni katika maisha ya kawaida wamejumuishwa katika visa vya tanzia. Kifo cha hao wahusika wote hata hivyo, huwa na athari ya huruma na woga kama katika tanzia asilia ya jadi. Matumizi ya mbinu hiyo katika uumbaji wa kazi za fasihi huwa na dhamira mahususi.

Labda ni muhimu kutaja hapa kwamba fasihi kama sanaa inayomhusu binadamu na mazingira yake, huelekezwa na itikadi, falsafa na miundo iliyoasisiwa ndani na nje ya jamii kulingana na nyakati na vipindi vya kihistoria. Njogu (1991) anaeleza ya kwamba kadri jamii inavyopiga hatua ndivyo fasihi nayo inavyochukua mkondo unaoafikiana nayo kwa kiasi fulani na yale yatukiayo katika jamii. Hivyo, jamii inavyobadilika ndivyo muundo wa tanzia na maudhui yake yanavyobadilika ili kubainisha taratibu, mitazamo na misimamo inayoenda ikibadilika kuhusu maisha ya binadamu.

Kuzaliza ni tukio la majaliwa na kifo ni jambo la lazima. Mwanadamu anastahili kuhurumiwa kwa maana hana hiari na hawezi kuzuia kuzaliwa kwake. Aidha, hawezi kujilaumu mwenyewe kwa kuzaliwa kwake wala kuwalaamu wazazi wake kwa kumzaa yeye. Nagg ambaye ni babake Hamm katika riwaya ya *Endgame* anasema ya kwamba: Isingekuwa mimi ingekuwa mtu mwingine yeyote. (*Endgame* uk.38) Beckett vilevile anaeleza ya kwamba hauwezi kumlaumu Mungu kwani kwake yeye haamini katika uwepo wa Mungu. Kwake maisha ni nguvu zisizoeleweka.

**Kifo kama Kikale**

Kikale ni taswira kongwe inayojitokeza mara kwa mara katika kazi ya fasihi. Aidha ni mhusika, motifu, ishara au taashira ambayo imekuwepo tangu zamani na inayojitokeza mara nyingi katika fasihi. Kulingana na maelezo ya Northrop Frye (1957) na Kamusi ya Longman (1987) kikale ni muundo asilia wa kitu ambao huigizwa na kufanya nakala za miundo ya vitu mbalimbali vinavyoundwa baadaye. Katika uchunguzi wake wa visasili mbalimbali kutoka kwa jamii za ulimwengu, Carl Gustav Jung (1933:1958) alibainikiwa ya kwamba kulikuwa na hadithi zenye taswira ya mashujaa wa ajabu wanaokufa na wenye nguvu za kiungu zinazoongoza wanadamu. Ubainikaji huu ulimpelekea Jung kuhitimisha kuwa tabia na mienendo ya binadamu huongozwa na sehemu ya ubongo ambayo inaitwa "ung'amuzi bwete" ambayo pia ilidhihirisha kuongozwa na imani zinazotokana au kirithiwa kutokana na visakale na dini. Hizi imani na dhana zilizorithiwa zilionyesha kupokezwa kutoka kwa kizazi kwenda kingine. Imani na dhana hizi hupatikana katika staarabu zote ulimwenguni katika nyakati mbalimbali za historia. Tukio hili linatokana na nguvu za vikale ambavyo huwa katika sehemu moja ya akili ya binadamu. Hivyo matendo na mienendo ya binadamu huongozwa na imani fulani ambazo zimerithiwa kutoka kwa visasili na kuhifadhiwa akilini. Kwa njia hii matendo ya watu mahsusi katika kipindi halisi cha wakati ni mwigo wa matendo ya awali yanayorekodiwa katika vikale.

Kulingana na Northrop Frye (1957), kuna hazina kubwa ya miundo, motifu, taashira na wahusika katika vikale ambavyo haviwezi kuwa miliki ya mwandishi mmoja. Wasanii wengine huchota sheria na mbinu hizi kutoka kwa vikale na huzitumia katika utunzi wao. Matumizi ya kifo katika kazi za sanaa yamedhihirika tangu nyakati za Aristotle hadi kwa nyakati za Shakespere na hivi sasa kifo

kinatumiwa katika kazi za sanaa na waandshi wengine. Northrop amefafanua kwamba kikale ni ishara au taashira ambayo huzua taswira inayojirudiarudia katika kazi ya sanaa kiasi kwamba inatambuliwa kama kiungo cha ujuzi wa mtunzi wa kazi fulani. Northrop analinganisha vikale na ulimwengu ambao unaangaliwa kama uwanja wa vitendo.Yafaa izingatiwe ya kwamba maana au hata kazi ya sanaa ni muundo wa kitaswira. Katika taswira ya vikale, ulimwengu unawakilishwa kijazanda ambapo kila kitu kina uwezo wa kufanana na kiingine. Matumizi ya kifo kama mbinu ya kutunga tamthilia ya Kiswahili vilevile unachukuliwa kuwa uwasilishaji wa kijazanda au kitaashira. Matumizi ya kifo katika tamthilia za Kiswahili yana uwezo mkubwa wa kufanana na matumizi ya kifo cha aina hiyo katika vikale au hata kazi zingine za awali. Bakhtin (1990) anaeleza ya kwamba historia ndio kiunganishi muhimu cha jana, leo na kesho. Umbo la fasihi lazima lieleweke katika muktadha maaalum wa kihistoria na wa kijamii. Ili kuiuielewa kazi ya fasihi ni muhimu kuielewa historia yake. Kikale kama ilivyoelezwa hapo juu ni taswira kongwe inayojitokeza mara kwa mara katika kazi ya fasihi. Taswira hii ina historia ya kujirudiarudia kama Frye anavyoeleza. Kuielewa taswira hii kunahitaji kuichunguza kama inavyojidhihirisha katika kazi za sanaa za vipindi mbalimbali vya historia. Hii ndiyo sifa mahsusi ya vikale. Matumizi ya kifo katika kazi za sanaa kama ilivyopita kuelezwa hapo juu yanaonyesha kujirudiarudia na yametimika kusawiri vikale vya aina mbalimbali.

Uhalisia huchunguza jinsi kitu fulani kinavyofanana na kile kinachojulikana. Kilichoandikwa kinapofanana na kilichojulikana, kinakuwa sanaa ya kitashbihi inayokusudiwa. Kama tashbiha ilivyo usawiri wa kisanaa wa uhalisia wa maisha kama inavyokusudiwa, ndivyo vikale vilevile vilivyo sanaa ya utambuzi wa jazanda inayokusudiwa. Katika vikale, misingi ya miundo ya kazi ya sanaa kwa mfano matumizi ya kifo hutambuliwa na kutengwa. Hamilton (1990) anaeleza kuwa uhakiki wa vikale ni uhakiki ambao huchukulia shairi kuwa igizo la mashairi na hivyo huchunguza sheria zinazokubalika, tanzu na vikale ambavyo huviunganisha. Kwa maneno ya Frye:

> "ushairi waweza kuumbwa tu kutokana na mashairi mengine, riwaya kutokana na riwaya nyingine." (Hamilton 1990:79)

Matumizi ya kifo katika tamthilia za Kiswahili lazima yawe yametokana na matumizi kama hayo katika tamthilia za tanzia za awali au katika vikale. Norhtrop Frye anaendelea kuelezea kuwa ni kupitia kwa utunzi wa tanzia za utamaduni wa Wagiriki kabla ya karne ya nne kabla ya kuzaliwa kwa masiha ambapo taashira za kifo zilijidokeza kwanza kisanaa. Ni katika misingi ya tanzia ya Kigiriki ambapo wasanii wa baadaye wameegemeza matumizi ya kifo katika kazi zao za fasihi. Kama ilivyo katika futuhi, kifo huchunguzwa vizuri zaidi katika tamthilia au katika drama. Hata hivyo si lazima tamthilia ya aina ya tanzia iwe na vitendo vinavyoishia na mikasa na vifo. Tamthilia zingine za tanzia huishia kwa furaha au mchanganyiko wa yote. Tamthilia iliyojaa matumizi ya kifo huwa na woga na majonzi. Asili ya matumizi ya aina hiyo katika sanaa lazima yatokane na msukumo wa mchezo au msuko wa matukio pamoja na vikale vipatikanavyo katika jamii.

Aghalabu katika tanzia na kinyume na futuhi ambayo hujishughulisha na wahusika ambao wako katika kikundi, tanzia huzingatia na kusisitisha matukio kwa mhusika binafsi wa kazi ya tamthilia. Basi uwezo wa mhusika wa kitanzia huwa kati ya ule wa binadamu wa kawaida na uwezo wa kiungu. Mhusika anayekufa katika tamthilia ya kitanzia huwa na uwezo wa juu zaidi akilinganishwa na binadamu wa kawaida. Uwezo wa wahusika hao hufikia ukingoni wanapofikia nguvu zilizowapita uwezo na ambazo hupatikana tu kwa Mungu, miungu, ajali, bahati, mahitaji ya lazima, majaaliwa, miktadha au muungano wa mambo hayo yote. Nguvu zozote ziwazo zile, wahusika wa tanzia huwa na wajibu wa kujenga daraja kati ya nguvu hizo na binadamu wa kawaida. Kwa mfano, Adam na Kristo ni wahusika ambao waliishi na walielea kati ya utukufu wa mbinguni na maisha ya kawaida ya duniani. Samson katika bibilia takatifu ambaye alikuwa na nuvu za kiunu aliharibu hekalu la Wafilisti naye mwenyewe akafa akiwa ndani yake katika kisa ambacho ni cha kitanzia. Visa na mikasa ya kitanzia ya wahusika mbalimbali katika bibilia vimeigizwa na watunzi wa baadaye wa kazi za sanaa kwa njia ya kujirudiarudia ya vikale.

Hata kama kifo cha mhusika kinatokea katika kazi ya tanzia inachukuana na kikale cha Kigiriki, cha Kikristo, cha Samson na Wafilisti, cha Adam au hakijulikani kinafanana na kikale kipi, kwa kawaida katika utunzi wa tamthilia na kazi zingine za sanaa huwa kuna mlinganisho wa kifo cha

mhusika ambacho kinalinanishwa na kingine kilichotokea awali kabisa na kinachoigiizwa. Kifo cha kitanzia katika katika kazi ya fasihi hubuniwa kisanaa ili kusababisha athari fulani ambayo hatimaye inaleta fundisho la kimaadili kwa hadhira.

Katika kiwango cha chini, sheria ambayo huongoza matumizi ya mauaji ya watu ya kikatili kwa wengine katika hali za kawaida za maisha ni ulipaji wa kisasi. Katika maisha yao, wahusika mashujaa hujenga uadui au kurithi hali ya uadui kutoka kwa watu wanaoishi nao. Wanapotangamana na watu, wale walioazimiana nao na ambao bado wanaweka kisasi dhidi yao, huchukua wakati wao kupanga mauaji ya watu fulani wanaochukuliwa kuwa maadui wao. Watu hao katika kazi za fasihi huumbwa kisanaa na huja kuwa mashujaa wa kitanzia. Muundo wa kazi ya sanaa unaotumia kifo kulipa kisasi huwa sahili. Kitendo asili kinachosababisha uadui hukamilika pale kisasi kinalipwa kwa kifo cha mhusika anayekisiwa kuwa adui. Ulipaji kisasi waweza kupangwa kupitia kwa miungu, mashetani na mapepo fulani ya kijamii au kwa njia yoyote ile inayochukuliwa kuwa inatoka katika ulimwengu wa pili. Katika uumbaji wa mhusika wa kitanzia anayepata kifo chake kupitia kwa njia ya kulipa kisasi kwa kosa alilolifanya au kwa sababu ya uadui, lazima kuwe na mbinu ya kufanya kisasi hicho kitoke katika ulimwengu wa pili kupitia kwa miungu, mashetani au mizimu alimradi nguvu zenyewe zitoke nje ya uwezo wa binadamu wa kawaida na zidhihirishe kwamba kama Yesu Kristo katika bibilia, mwanadamu hana nguvu za kuibadilisha hatima yake. Mfano ni hadithi ya mhusika kwa jina Elosini kutoka Afrika magharibi ambaye tangu kuzaliwa kwake, hatima yake ilikuwa kutolewa matoleo ya kikafara.

Ni muhimu kuzingatia ya kwamba kifo kinapompata mhusika wa tanzia, kifo hicho huzua hali ya kijazanda katika kazi ya sanaa. Northrop (ameishatajwa) anaeleza jazanda kama mbinu ya mtu, dhana au kitu kueleweka zaidi ya jinsi hali ilivyo. Ni mbinu ambayo katika fasihi hutumika katika kusema machache na kumaanisha mengi iwezekanavyo. Vilevile, ni mfumo wa kusema maneno ambayo hayalengi maana yake moja kwa moja. Kifo cha mhusika katika tamthilia za Kiswahili kinapotokea, inatarajiwa kwamba maana yake imefichika na kina uwezo wa kuwa zaidi ya kilivyofanyika.

Kitendo ambacho husababisha kifo huanza kwa matendo ambayo ni kinyume na maadili ya jamii. Matendo hayo ambayo ni dhambi au makosa ambayo yanatokea katika maisha ya mhusika wa tanzia, yaliitwa na Aristotle "hamartia" au "tragic flaw". Kifo cha kitanzia husababisha woga na huruma kwa hadhira na wakati mwingine huwafanya kutokwa na machozi. Woga na huruma ambao huwajia watazamaji wa mchezo wa kuigiza ni hisi tu kimtakaso za kimaadili. Lakini kwa vyovyote woga au huruma huo, hauna uhusiano na hali inayosababisha kifo hicho katika kazi ya fasihi bali huwa ni athari ya mkaso hisia kwa watazamaji wa mchezo wa kuigiza.

Nadharia ya Aristotole kuhusu tanzia imeanzishwa kwa misingi ya utunzi wa *Oedipus Tyranus* na tamthilia ya Hegel ya *Antigone*. Northrop akitoa mfano anaeleza ya kwamba baada ya kuona kikale cha tanzia ya mwanadamu katika hadithi ya Adamu, mwandishi Milton alikubaliana na tamaaduni za dini ya Kikristo na ya Kiyahudi na maelezo yanayotolewa kuhusiana na hadithi ya Adam. Shujaa Adam alikuwa na uwezo wa kufanya uamuzi kuhusu hatima yake. Lakini katika hali ya kujisahau na kutupilia mbali uwezo wa kuchagua hatima yake, Adam alichagua kifo na kuanguka. Hivyo Milton aliunganisha aina mbili za vikale ambavyo ni kikale cha tanzia ya urasmi na kikale cha tanzia ya Kikristo pale anapoandika kuhusu kuanguka kwa shetani kutoka mbinguni.

**Hitimisho**

Katika makala haya, nimeweza kuchunguza matumizi ya tukio la kifo katika utunzi wa kazi bunifu za fasihi hasa katika tamthilia. Ilibainika kwamba kifo ni motifu kongwe inayojirudia katika kazi za fasihi na ambayo huchotwa na watunzi mbalimbal ili kuwawezesha kubuni kazi zao. Tukio la kifo lilikuwa na umuhimu mkubwa kwa watunzi na hasdhira yao kwani kiliweza kutumiwa kibunifu ili kujenga na kuendeleza umbo la kazi za sanaa na dhamira zao. Matumizi ya kifo katika utunzi wa kazi za fasihi yamekumbwa na mabadiliko ya kiwakati jinsi wakati unavyoenda ukibadilika. Utafiti huu uluthibitisha kwamba matumizi ya kifo ni mbinu mwafaka inayotumiwa na wasanii katika kuimarisha dhamira na ujumi wa kazi zao za fasihi.

**Marejeleo**

Allen, J. W. T.(1971). *Tendi*. London – Great Britain: Richard Clay (The Chancer Press) Ltd

Bakhtin, M. M. (Ed) (1990). *Art and Answerability*. Austin: University of Texas Press.

Beckett, S. (1956). *Waiting for Godot*. London: Faber and Faber Ltd.

Cruickshank (1958). *Albert Camus: the literature of Revolution*. London: Oxford University Press

Cuddon, J. A. (1977). *A Dictionary of Literary Terms*. London: Andre Deutsch Ltd.

Durkheim, E. (1957). *Suicide: A Study in Sociology*. New York: Free Press.

Fowler (1976). *Concise Oxford Dictionary*. Oxford University Press

Hamilton, A. C. (1990). *Northrop: Anatomy of his Criticism*. Toronto: Toronto University Press.

Indagasi, H. (1991). *Notes on William Shakespear's Romeo and Juliet*. Nairobi: East African Educational Publishera Ltd.

Ionesco, E. (1962). *Rhinocerous/ The chairs the Loss on Harmondsworth*. Penguin.

Plaks, A.H (1976). *Archetype and Allegory in The Dream of the Red Chamber.* Princeton and Guildford, Survey: Princeton University Press.

Merriam, G. and C co. (1971). *Webster's Savent New Collegiate Dictionary*. London: G. Bell and Son Ltd.

Muindi, A. (1990). "Usawiri wa Wahusika Makhaba katika riwaya ya Said Ahmed Mohamed". Tasnifu ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mushi, S. S. (1971). *Mfalume Edipode*. Nairobi: Oxford University Press.

Northrop, Frye (1957). *Anatomy of criticism: Four essays.* Princeton, New Jersey: Princeton University Press.

Rene Wellek na Austin Waren (1949). *Theory of Literature*. USA, Great Britain: Penguin Books

Roderick, W. (1986). *The Merchant of Venice.* Between Towns Road, Oxford: Macmillan Publishers

Sage, J. (Mhariri). (1962). *A Dictionary of Symbols.* Cirlot, J.E (Mwandishi). London: Routledge and Kegan Paul Publishers.

Senkoro, F. E. M. K. (1983). *Fasihi.* Dar es Salaam. Press and Publicity Centre.